



18/04/2024

**TANGAZO LA AJIRA ZA WAANDISHI WASAIDIZI NA WAENDESHAJI WA
VIFAA VYA BAYOMETRIKI (BVR KIT OPERATORS)**

Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Ifakara imepokea barua yenye Kumbukumbu Na. SAB.74/75/01/20 ya tarehe 15/04/2024 kutoka kwa Mkurugenzi wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Tanzania inayohusu Ajira za Waandishi Wasaidizi na Waendeshaji wa Vifaa vya Bayometriki kwa Madhumuni ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Kwa barua hiyo, Mkurugenzi wa Uchaguzi anawaalika wenye sifa kuomba nafasi hizo kwa kurejea Matangazo ya Kazi yaliyobandikwa kwenye mbao za matangazo za Ofisi za Watendaji Kata, Mitaa na Vijiji kuanzia tarehe 18/04/2024 hadi tarehe 27/04/2024.

Tangazo hilo la nafasi za kazi za muda limetaja Sifa za Mwombaji wa Nafasi ya Mwandishi Msaidizi, Sifa za Mwombaji wa Nafasi ya Mwendeshaji wa Vifaa vya Bayometriki, Malipo ya Kazi, na Masharti ya Jumla ya Mwombaji.

MAELEKEZO MUHIMU YA KUZINGATIA

1. Mwombaji awasilishe maombi yake kwa kubainisha kazi anayoomba kama ni Mwandishi Msaidizi au Mwendeshaji wa Kifaa cha Bayometriki.
2. Mwombaji athibitisha ukaazi wake kwenye Kata husika kwa kupata uthibitisho kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji au Mtaa
3. Mwombaji ambaye ni Mtumishi wa umma apitishie barua yake ya maombi kwa mwajiri wake
4. Mtendaji wa Kata atapokea Maombi yote ya barua bila kufungua barua za maombi na ataziwasilisha kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Ifakara tarehe 28/04/2024

Tangazo hili limetolewa na;


Zahara M. Michuzi

MKURUGENZI WA MJI IFAKARA





JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI



TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA ZA WATENDAJI WA
VITUO VYA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA
WAPIGA KURA

Kwa madhumuni ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 7 (4) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024 Mkurugenzi wa Uchaguzi anakaribisha maombi kutoka kwa wataanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za waandishi wasaidizi na waendeshaaji wa vifaa vya bayometriki.

A. SIFA ZA MWOMBAJI WA NAFASI YA MWANDISHI MSAIDIZI

- (a) awe ni raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi;
- (b) awe amehitimu elimu ya kidato cha nne au zaidi na anajua kusoma na kuandika katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza;
- (c) awe mwenye ujuzi wa kutumia kompyuta au simu janja (Smartphone);
- (d) awe ni mkazi wa mtaa au kijiji katika kata anayoomba kuwa mwandishi msaidizi;
- (e) asiwe kiongozi au kada wa chama cha siasa; na
- (f) awe ni mwadilifu na mtiifu.

B. SIFA ZA MWOMBAJI WA NAFASI YA MWENDESHAJI WA VIFAA VYA BAYOMETRIKI

- (a) awe ni raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi;
- (b) awe amehitimu elimu ya kidato cha nne au zaidi na anajua kusoma na kuandika katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza;
- (c) awe mwenye ujuzi wa kutumia kompyuta au simu janja (Smartphone);
- (d) awe ni mkazi wa mtaa au kijiji katika kata anayoomba kuwa mwendeshaaji wa kifaa cha bayometriki;
- (e) asiwe kiongozi au kada wa chama cha siasa; na
- (f) awe ni mwadilifu na mtiifu.

C. MALIPO

Malipo yatakuwa kama ifuatavyo: -

- i. Kwa siku za uboreshaji wa Daftari vituoni waandishi wasaidizi na waendeshaaji wa vifaa vya bayometriki watalipwa posho ya Shilingi 50,000/= kwa siku na nauli Shilingi 10,000/=.
- ii. Wakati wa mafunzo, waandishi wasaidizi na waendeshaaji wa vifaa vya bayometriki watalipwa posho ya Shilingi 50,000/= na nauli Shilingi 10,000/= kwa kila siku ya mafunzo.

D. MASHARTI YA JUMLA


- i. Mwombaji lazima aainishe nafasi anayoomba pamoja na kata anayoomba kufanyia kazi.
- ii. Mwombaji aambatishe: -
 - a. nakala ya vyeti vya Elimu ya Sekondari na Taaluma vinavyohitajika kulingana na kada husika kama vilivyofafanuliwa katika Tangazo hili.
 - b. wasifu (CV) ukionesha anuani yake ya makazi, namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini wake wawili.
 - c. picha mbili zenye ukubwa sawa na picha iliyomo kwenye pasi ya kusafiria (Passport size) za hivi karibuni.
 - d. barua ya utambulisho kutoka kwa mtendaji wa serikali ya mtaa au kijiji katika eneo analoishi.
- iii. Mwombaji ambaye ni mtumishi wa umma apitishie barua yake ya maombi kwa mwajiri wake.

**MWOMBAJI ATAKAYEBAINIKA KUWASILISHA TAARIFA ZA KUGHUSHI
ATACHUKULIWA HATUA ZA KISHERIA.**

Barua zote za maombi ziandikwe kwa anuani ifuatayo: -
Mkurugenzi wa Uchaguzi,
Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi,
Uchaguzi House,
Enco la Uwekezaji Njedengwa,
Kitalu D, Kiwanja Na.4,
5 Barabara ya Uchaguzi,
S.L.P. 358,
41107 DODOMA.

ILI KURAHISISHA UTUMAJI WA MAOMBI, BARUA ZOTE ZIKIWA
ZIMEFUNGWA ZIPELEKWE KWA MTENDAJI WA KATA AMBAYE
ATAZIPOKEA NA KUZIWASILISHA KWA MKURUGENZI WA
HALMASHAURI

MWISHO WA KUWASILISHA MAOMBI NI TAREHE 27 APRILI, 2024

Limetolewa na: 
Kallima, R.K.
MKURUGENZI WA UCHAGUZI
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI
DODOMA.
15 APRILI, 2024

